
# Miaka 25 ya REPOA Kujenga Uwezo wa Utafiti na Kuchangia Sera za Maendeleo

Katika miaka 25 iliyopita tangu kuanzishwa kwake mwaka1995, REPOA imejitokeza kuwa taasisi mahiri ya utafiti nchini Tanzania na ya upekee wa namna ilivyotoa mchango kwenye kujengea watafiti uwezo wa kufanya tafiti za kisera na pia kwa watumiaji mbali mbali wa tafiti. Tafiti za kisera ni muhimu sana katika mijadala ya kisera za umma na katika mipango ya maendeleo duniani. Ushahidi wa hoja hii unaonekana katika nchi zilizoendelea, ambapo kati ya taasisi za utafiti kama REPOA zaidi ya 11,000, karibu nusu yake ziko katika nchi hizo. Afrika chini ya jangwa la Sahara ina 6% tu ya hizo taasisi. Kama ilivyo kwa nchi zingine za Afrika, Tanzania zipo taasisi chache sana za aina hii, ikijumuisha taasisi huru za utafiti, vitengo za utafiti ndani ya vyuo vikuu, na taasisi za umma za utafiti wa kisekta. REPOA ni moja kati ya taasisi chache zilizo huru za utafiti ambazo zimejihusisha kwa karibu sana na mabadiliko ya kisera Tanzania na katika dhana nzima ya maendeleo tangu ilipoanza majukumu yake mnamo mwaka 1995.

Ikifanya kazi kwa karibu na watafiti washirika, taasisi washirika, na wanufaika wa kazi zake, ikisaidiwa na wafadhili mbalimbali kwa miaka 25, REPOA imetoa mchango mkubwa katika juhudi za taifa katika kujenga uwezo wa kufanya tafiti za kisera, kuongeza matumizi ya ushahidi katika uandaaji wa sera, na kuhimiza mijadala ya kisera ikishirikisha wadau mbali mbali. Makala hii inatoa muhtaasari wa matokeo mapana matatu yatokanayo na shughuli za REPOA, kati ya matokeo mengi katika miaka 25 iliyopita.



**Mkurugenzi Mtendaji wa REPOA, Dk. Donald Mmari akiagana na aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, baada ya kuzindua kongamano la kimataifa la 24 mnamo tarehe 10 Aprili , 2019 jijini Dar es Salaam. Nyuma yake ni aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu katika Wizara ya Elimu, Dk. Maria Semakafu na Balozi wa Norway nchini, Mheshimiwa Elisabeth Jacobsen. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa sasa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

**Kujenga Uwezo wa Utafiti na Uchambuzi wa Kisera**

Wakati REPOA ikianzishwa, changamoto kubwa ya kisera ilikuwa kuendelea kwa umaskini, pamoja na juhudi za serikali tangu uhuru na maboresho ya kisera ya miaka ya 1980 na 1990. Kwenye ufunguzi wa warsha ya utafiti juu ya umaskini iliyofanyika tarehe 11 Januari 1994, Waziri wa Sayansi, Teknologia na Elimu ya Juu wa wakati huo, Hayati Benjamin William Mkapa alisema sababu mojawapo ya kuendelea kwa umaskini inaweza kuwa, wakati mikakati ya serikali ilikuwa na malengo mazuri na ilihitajika, msingi wake haukuwa mzuri na utekelezaji unaweza kuwa ulifanywa kwa haraka sana. Alishauri, kama inavyonukuliwa kwenye hotuba yake, "...kumekuwepo, na kumeendelea kuwepo, utafiti haba kama msingi wa mipango na mikakati ya kuondoa umasikini inayofanywa na serikali, mashirika yasio ya kiserikali, na wafadhili kwenye nchi zinazoendelea kama nchi yetu". Kwa hiyo ilionekana kuwa utafiti juu ya namna ya kuondoa umaskini ni muhimu ili kuwa na sera na mikakati ya muda mrefu na endelevu katika kuondoa umaskini. Haya pia yalisemwa vizuri katika hotuba ya Bwana J.Yzermans, Ofisa Mwandamizi katika Ubalozi wa Uholanzi Dar es Salam, na kunukuliwa ".. lengo la mpango huu mpya wa utafiti ni kuweka utafiti katika mpango mahususi na kushughulika na changamoto ya uwezo mdogo wa kiutafiti ndani ya nchi juu ya changamoto za maendeleo kwa muda mrefu kwa kutumia mfumo thabiti wa kitaasisi".

Jukumu la kwanza la REPOA wakati wa kuanzishwa kwake ilikua ni kujenga, kuimarisha, na kuendeleza uwezo wa ndani wa kufanya utafiti na kujenga desturi ya kitaaluma ya kuandaa ajenda ya utafiti huru juu ya namna ya kuondoa umaskini Tanzania. Programu ya REPOA ya kujenga uwezo wa watafiti ilihusisha aina mbili: mafunzo kwa vitendo na mafunzo mahsusi. Aina ya kwanza ilihusisha kutoa fedha kwa watafiti kwa njia ya ushindani wa wazi. Katika mfumo huu, watafiti wachanga walishawishiwa kuungana na watafiti waandamizi ili waweze kujifunza kutoka kwao, pamoja na ushauri na usimamizi wa karibu katika ngazi zote za utafiti. Mfumo thabiti wa kusimamia ubora, ikiwamo semina za wazi, wahakiki huru wasiojulikana na watafiti, na usimamizi wa jumla chini ya kamati ya kifundi ya ushauri. Utaratibu huu uliimarisha sana uwezo wa watafiti na kuhakikisha kuwa ripoti za utafiti zilikuwa na kiwango cha juu, na hivyo kuchapishwa katika majarida na kutumika katika mihadhara na semina mbalimbali, ikiwemo mikutano ya utafiti inayoandaliwa na REPOA kila mwaka. Mada kuu za utafiti katika miaka mitano ya kwanza ya REPOA zilikuwa ni mahusiano kati ya umaskini na sera za umma; mahusiano kati ya umaskini na mazingira; mchango wa teknologia katika kuongoa umaskini; masuala ya kijinsia katika umaskini; na viambishi vya umaskini vinavyotokana na desturi za jamii. Mada hizi za utafiti zimekuwa zikibadilika kila baada ya miaka mitano kwa kuakisi mabadiliko ya kiuchumi na miundo ya kijamii pamoja na mabadiliko ya kisera nchini, na pia kuzingatia sababu zingine za mabadiliko katika ngazi za kikanda na dunia kwa ujumla.

Mafunzo-mahsusi yalitolewa kwa watafiti na wachambuzi wa masuala ya kisera kwenye maeneo ya mbinu za utafiti, uchambuzi wa takwimu, na ujuzi wa uandishi. Kadiri muda ulivyokwenda, kujenga uwezo wa watumaiji wa takwimu kwenye maeneo kama uchambuzi wa bajeti na ufutialiaji wa matumizi ya umma ulikuwa sehemu muhimu ya mafunzo ya REPOA. Uzoefu wa REPOA katika kujenga uwezo ulipelekea kuanzishwa kwa programu ya stashahada ya uchambuzi wa kisera, ikiwa ni ushirikiano wa REPOA, ESRF, na Taasisi ya Mafunzo ya Kijamii ya Uholanzi (kwa sasa ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Erasmus, Rotterdam). Programu hii ilifadhiliwa na Shrika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kwa miaka minane, ikifaidisha wataalam waliokuwa katika hatua za mwanzo na kati katika taaluma zao. Wengi wa wanufaika wa juhuzi za REPOA za kujenga uwezo leo hii wana mafanikio katika taaluma na majukumu yao kwenye taasisi za elimu ya juu, mashirika ya kimataifa, taasisi zisizo za kiserikali, na serikalini. REPOA imeendelea kutoa mafunzo mahsusi kama sehemu ya programme za utafiti, kama vile namna ya kukusanya tafiti za msingi kwa kutumia teknolojia mpya. Pia kumekuwa na mafunzo mengine kwa watumiaji wa tafiti, yakiwa na lengo la kuimarisha uhisiano kati ya tafiti na sera, kama vile mafunzo ya namna ya kutumia ushahidi utokanao na tafiti kuandaa au kupitia sera yaliyoanzishwa mwaka 2019, yakilenga zaidi wachambuzi wa sera, na mafunzo kwa wanahabari juu ya matumizi ya takwimu na usambazi wa taarifa kwa kutumia takwimu.

**Mchango Kwenye Changamoto za Kisera na Mijadala ya Maendeleo ya Kimataifa**

Katika nchi yotote, mwelekeo wa maendeleo na sera zake huwa zinaongozwa na mchanganyiko wa hali za ndani ya nchi pamoja na ushawishi utokanao na mazingira ya kiuchumi na kisiasa duniani. Haya yote yamekua yakibadilika sana tangu Tanzania ipate uhuru mwaka 1961 na ndivyo mfumo wa kisera umekuwa ukibadilika: kutoka kukuza uchumi na maendeleo miaka ya 1960; uzalishaji na upatikanaji wa mahitaji ya msingi miaka ya 1970; sera za soko huria kupitia mageuzi ya kimuundo miaka ya 1980; kutokomeza umaskini miaka ya 1990; na kukuza uchumi, biashara, na maendeleo katika miaka ya hivi karibuni. Kuzaliwa kwa REPOA kulishabihiana na Mkutano wa Copenhagen wa 1995 na baadae Mpango wa Kina wa Maendeleo wa Benki ya Dunia wa 1999, ambapo pia yalifuata Malengo ya Maendeleo ya Milenia ya miaka 2000.

Wasiwasi wa kuwepo kwa madeni yasiyovumilika ulipelekea kuanzishwa kwa utaratibu wa kupunguza madeni kwa nchi zinazoendelea zenye madeni makubwa, kwa masharti ya kuandaliwa kwa mikakati ya kupunguza umaskini kuanzia mwaka 2001. Nchini Tanzania, msisitizo kwenye mpango wa mabadiliko ya kimfumo ulianza kupungua, na mkazo ukaelekea kwenye Mkakati wa Kitaifa wa Kuondoa Umaskini wa mwaka 1997, na Dira ya Maendeleo 2025 ulioandaliwa mwaka 1999. Mkakati wa 1997 ulikuwa mkakati wa muda wa kati ulioainisha visababishi vya umaskini na hatua za kisera za kufikia malengo ya ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato kwa 50% ifikapo 2010. Dira ya taifa ya maendeleo ilizungumzia nia ya kutomeza kabisa umaskini uliokithiri na kufikia uchumi wa kiwango cha kati ifikapo mwaka 2025. Kwa mara nyingine, ni rahisi kuona kuwa kuanzishwa kwa REPOA kulitokea sanjari na mtazamo mpya wa kisera juu ya umaskini, na ndio wakati ambao utafiti juu ya nyanja mbalimbali za umaskini ulitiliwa mkazo sana.

Mkakati wa Kupunguza Umaskini Tanzania uliambatana na Mfumo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji Umaskini ulioanza mwaka 2001, mfumo ambao ulitoa fursa kwa utafiti na uchambuzi huru na ulitenga fedha za utafiti huo ili usaidie katika utekelezaji wa mkakati wenyewe. Shughuli za utafiti na usimamizi wa fedha za utafiti zilisimamiwa na Kamati ya Utafiti na Uchambuzi ambayo ilikuwa sehemu ya mfumo wa kitaifa wa ufuatiliaji, na REPOA ilikuwa ndio Sektrariati ya kamati hiyo. Matokeo ya tafiti zake zilisaidia kupima utekelezaji wa mkakati katika kufikia malengo yake na kutoa mapendekezo ya mabadiliko ya kisera pamoja na mikakati iliyohitajika kuongeza ufanisi. Vipaumbele za utafiti viliafikiwa kwa ushirikishwaji wa wadau wote, jambo lililofanya tafiti zake kuwa na manufaa sana, na matokeo yake yalihuisha sana kuimarishwa kwa sera mbali mbali. Moja ya matokeo ya kazi za kamati hii Ripoti za Umaskini na Maendeleo ya Watu zilizotolewa kila baada ya miaka miwili. Ripoti ya kwanza ya mwaka 2002, ilitoa picha ya hali ya umaskini nchini kwa kuangalia kila kiashiria na hatua iliyofikiwa kuelekea kwenye malengo, hali ya umaskini katika maeneo tofauti kwa jiografia ya nchi, umaskini wa mijini, na mahusiano kati ya uchumi wa jumla na uchumi wa mdogo mdogo. Ripoti hiyo ilishauri kuwepo tathmini ya kina ili kuelewa ukuaji na ubora wa uchumi wetu, pamoja na njia za kufanya ukuaji wa uchumi kuwa na nguvu ya kupunguza umaskini na hali tete za watu. Majadiliano yaliyotokana na ripoti hii pia yalichagiza mchakato wa uaandaji wa mkakati wa pili wa kupunguza umaskini ambao ulijikita pia kukuza uchumi, na hivyo mkakati uliofuata ukaitwa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA). Mkakati huu ulikua na nguzo tatu, ambazo ni uchumi na umaskini wa kipato; ubora wa maisha na ustawi wa jamii; na utawala na uwajibikaji. Programu ya utafiti ya REPOA (2004-2009) ilijikita kuangalia namna ya kuondoa umaskini ndani ya wigo mpana wa mahusiano kati ya ukuaji wa uchumi; kilimo na mazingira; mazingira magumu na uhifadhi wa jamii; na masuala ya kijamii, kisiasa, na desturi. Pia maeneo ya utawala, teknologia, na jinsia yalibaki kuwa maeneo muhimu ya jumla katika tafiti zake. Tafiti za REPOA ziliendelea kujikita katika kuainisha maeneo ya kisera katika kutambua vikwazo vya ukuaji uchumi, namna ya kukuza tija na ubora wa uchumi, namna ya kuboresha mchango wa uhifadhi ya jamii ili kuchagiza mabadiliko, na kuhimiza mageuzi ya kiutawala ili kuimarisha uwajibikaji na huduma za jamii kama namna endelevu za kupunguza umasikini. Tafiti hizi ziliendeleza msukumo wa ukuaji wa uchumi kuwa sehemu kuu ya mikakati ya maendeleo kama njia endelevu ya kupunguza umaskini.

Waandishi wahabari waandamizi wakifuatilia mafunzo yaliyoandaliwa kwa ajili yao ili kujifunza namna bora ya kuandika matokeo ya tafiti zinazotolewa na REPOA.

Tafiti zilizofuata zilitoa mwanga juu ya mfumo ya uchumi wa vijijini, ajira na tija, mabadiliko ya muundo wa idadi ya watu, na dhana ya muunganiko kati ya sera za kiuchumi na zile za kijamii. Uelewa wa undani zaidi juu ya dhana ya ukosefu wa jumla wa usalama wa kiuchumi, na kukua kwa uchumi usio rasmi ulichagiza mawazo mapya juu ya namna ambavyo hifadhi za jamii unaweza kuchangia katika kuleta mabadiliko kwa kuongeza uwezo wa watu pamoja na mifumo ili kuongeza umahiri wenye tija. Mwaka 2009,

tafiti zingine ziliibua mjadala mpya juu ya sera mahsusi za kukuza uchumi, hususan juu ya jukumu la dola katika mazingira ya uchumi wa soko huria. Mapendekezo la msingi juu ya dola yenye msukumo wa maendeleo ni umuhimu wa kuwa na dira iliyofafanuliwa wazi, mkakati wa maendeleo wa muda mrefu, kudumisha utulivu katika uchumi wa jumla na kuhakikisha utawala bora, pamoja na uongozi imara wa kisiasa na watumishi wa umma wenye sifa thabiti. Mkakati wa pili wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA II) wa 2010/11-2014/15 na Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/12-2015/16 ilibeba baadhi ya hivi vipengele, yote ikianisha umuhimu wa taasisi imara pamoja na sekta binafsi, utawala bora, ufanisi wa kiuchumi ukichagizwa na uwekezaji wa umma kwenye miundombinu ya msingi, pamoja na ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Vipengele hivi pia vilijitokeza katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21).



**Aliyekuwa Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dk. Phillip Mpango akijibu maswali ya waandishi mara baada ya Kufungua kongamano la 22 lililoandaliwa na REPOA tarehe 29 Machi, 2017. Nyuma yake ni Dk. Donald Mmari, Mkurugenzi Mtendaji wa REPOA, na Meja Jenerali Mstaafu Profesa Yadon Kohi, Mwenyekiti Mstaafu wa Bodi ya Wakurugenzi ya REPOA. Mheshimiwa Dk. Phillip Mpango kwa sasa ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

Katika miongo miwili iliyopita, uchumi wa Tanzania umekua na umehimili ukuaji chanya wa uchumi. Hata hivyo, wasiwasi juu ya muunganiko hafifu kati ya ukuaji wa uchumi na kupungua kwa umaskini umeendelea kutawala majadiliano ya kisera, jambo ambalo limechagiza mtazamo kuwa madaliko katika muundo wa uchumi ni muhimu kwa maendeleo jumuishi. Ilionekana kuwa eneo kubwa la kuwakomboa watu kutoka kwenye umaskini ni kubadili muundo wa kilimo na uchumi wa vijijini, ambapo wananchi wengi wanaishi na kupata riziki zao. Lakini hii siyo changamoto mpya kwa kuwa uongozi wa nchi tangu uhuru ulijaribu kupambana nayo kwa kutumia mageuzi mbalimbali ya kisera. Changamoto ya namna ya kubadili kabisa muundo wa kilimo na uchumi wa vijijini unaendelea kuwa ajenda muhimu kwenye tafiti za REPOA. Lengo ni kufanikisha azma ya kuwa na sekta ya kilimo yenye tija kubwa kwenye uzalishaji na iliyoshindani katika masoko ya ndani na nje, ikiongozwa na wakulima wadogo wakishirikiana na wakulima wakubwa chini ya mfumo mzuri wa uratibu. Tafiti zilizofanywa katika minyororo kadhaa ya thamani kama vile kahawa, sukari, korosho, katani, na mboga zinaonyesha kuwa mageuzi katika kilimo yanawezekana kupitia ubunifu kwenye mifumo ya kitaasisi na kiuratibu inaoweza kundoa vikwazo vya kukuza tija kwenye sekta, kushusha gharama, kuwezesha matumizi ya teknologia sahihi kwa ufanisi katika uzalishaji, na kuwaunganisha wakulima kwenye minyororo ya thamani iliyoshindani.

Programu ya sasa ya utafiti wa REPOA inaendeleza uchambuzi wake wa awali, ikijikita kwenye kuangalia visababishi vya mageuzi yenye ufanisi, ikiwa ni pamoja na matumizi ya kimkakati ya rasilimali; ujuzi na ajira; mazingira ya kisera na kitaasisi kwa ajili ya kuimarisha ushindani katika sekta za uzalishaji, zikiwemo kilimo, viwanda, na biashara; kukabili changamoto ya uchumi usio rasmi; utawala jumuishi na unaowajibika katika kuleta usawa na uwazi; ushiriki wa wananchi na maendeleo ya kiuchumi katika ngazi za mitaa; hifadhi imara ya jamii na usawa wa kijinsia; mazingira, na teknologia. Maeneo haya yote ni muhimu, wakati taifa likiaandaa Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Miaka Mitano, na muhimu zaidi kuendeleza kasi kuelekea kwenye viwango vya juu zaidi vya uchumi wa kati.

Maboresho ya Serikali za Mitaa, Kuongeza Ushiriki wa Wananchi, na Maendeleo ya Uchumi katika ngazi za Mitaa

Ajenda ya Maboresho ya Serikali za Mitaa nchini Tanzania ilianza mwaka 1996, ikilenga kuimarisha mahusiano kati ya serikali kuu na serikali za mitaa katika muktadha mpana wa maboresho ya sekta ya umma kwa ajili ya kuboresha huduma kwa umma. Ajenda hii ya maboresho ilitafsiriwa kwenye chapisho la Ugawanyaji wa Madadaka la mwaka 1998, chapisho ambalo lilipendekeza mfumo wa ugatuzi uliotekelezwa chini ya Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa. Maboresho haya yalilenga ugatuzi kwenye maeneo ya kisiasa, utawala, na uwezo wa kufanya uamuzi kwenye masuala ya fedha. Kuendana na sera ya ugatuzi, REPOA ilianza utafiti juu ya serikali za mitaa na utoaji wa huduma za jamii katika miaka ya mwisho ya 1990, na baadae ikaanza programmu ya utafiti juu ya maboresho ya serikali za mitaa ikishirikiana na taasisi ya Chr. Michelsen Institute (CMI) ya Norway, kuanzia mwaka 2002 mpaka 2012. Tafiti hizi zilitoa mchango mkubwa kwenye tathmini na utekelezaji wa maboresho ya serikali za mitaa katika awamu zote mbili za programu, na zilitoa mrejesho na mafunzo yaliyotokana na hatua mbalimbali za utekelezaji wa maboresho.

Maamuzi ya kisera ya baadhi ya serikali za mitaa, na mahusiano kati ya utawala na uwajibikaji ni baadhi ya maeneo yalifofaidika na matokeo ya tafiti za REPOA, na bila shaka tafiti za watu na mashirika mengine zilichangia. Tafiti zilielezea vizuri vyanzo vya nguvu na michakato ya kitaasisi ilivyokuwa msingi wa mchakato wa bajeti na mipango shirikishi katika ngazi za kata na mitaa. Tafiti zilizoendelea kwenye eneo hili ziliendelea kutoa matokeo na taarifa kwa serikali na taasisi zisizo za kiserikali juu ya ugatuzi wa madaraka, zikionyesha zimefanikiwa wapi na changamoto zipi zimebaki ambazo zingehitaji kuimarishwa kwenye utekelezaji au kufanyiwa mapitio ya sera. Serikali ilipokea vizuri mapendekezo na kuchukua hatua kadhaa zenye malengo ya kuongeza ushiriki wa wananchi katika ngazi za mitaa, kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi, na kuchagiza juhudi za kuimarisha maendeleo ya kiuchumi katika ngazi za mitaa. Juhudi hizi ni pamoja na mapitio na mashauriano ya sera ya ugawanyaji wa madaraka na Mpango wa Kuimarisha Mikoa na Serikali za Mitaa.

**Hitimisho**

Makala hii inatuonyesha mambo mawili makubwa ambayo mara nyingi yanapewa uzito mdogo au kupuuzwa. Kwanza, utafiti unaoaminika na wenye umuhimu una sehemu kubwa katika michakato sahihi wa maendeleo. Pili, katika miongo miwili iliyopita, tafiti zimetoa mchango mkubwa kwenye mapitio na maandalizi ya sera na mikakati ya maendeleo kuliko miaka ya nyuma, na zimesaidia sana kuwa kiungo kati ya sera za serikali na mahitaji ya wananchi. Mchakato wa maandalizi ya sera inaendelea kuzingirwa na msukumo mkubwa zaidi kutokana na nguvu za utandawazi, mabadiliko ya utawala wa dunia na siasa za kiuchumi, pamoja na mabadiliko ya kasi ya teknolojia. Yoye haya yanahitaji sana kuziba pengo kati ya tafiti kwa upande mmoja, na ubora na ufanisi wa sera kwa upande mwingine. Kuzuka kwa janga la corona na usumbufu utokanao na janga hilo kwenye shughuli za kiuchumi na madhara ya kiafya na ustawi wa jamii, huenda kukasababisha utaratibu mpya wa mahusiano ya kiuchumi na kijamii duniani ambao utaleta changamoto na fursa mpya. Baadhi ya changamoto ni ukuaji hafifu wa uchumi, kuongezeka kwa tofauti za vipato baina ya watu na jamii, umaskini, na ugumu wa mazingira ya watu kiuchumi na kijamii. Baadhi ya fursa ni pamoja na kuibuka kwa masoko mapya, uwezekano wa kupanua biashara kati ya kanda barani Afrika, na uzalishaji wa ndani wa madawa na vifaa tiba.

Kupanuka kwa kasi na wigo wa upatikanaji wa taarifa, kuongezeka kwa mahitaji ya uwazi, na kuongezeka kwa ugumu wa kutengeneza sera katika mazingira yanayobadilika, makubaliano kadhaa ya kikanda na kimataifa, kuongezeka kwa matakwa ya wananchi kwa viongozi waliochaguliwa na watumishi wa uma kukidhi matokeo tarajiwa ya maendeleo, na umuhimu wa kutoa taarifa sahihi na kwa wakati, kwa pamoja vitahitaji utafiti zaidi na ushahidi ili kuzifanya hatua mbalimbali za kisera kuwa na matokeo chanya na ziweze kulenga kufikia matarajio ya wadau tofauti.

REPOA imejibu vizuri mahitaji ya sera na maendeleo ya watanzania kulingana na uhalisia wa maendeleo ya nchi kwa nyakati tofauti, pamoja na matarajio yatokanayo na ajenda za maendeleo ya kikanda na dunia kwa ujumla, kama Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Ajenda ya Umoja wa Africa 2063, na Maendeleo Endelevu ya Milenia 2030. Kwa kuthibitisha umahiri wa REPOA katika utafiti na mchango wake, utafiti wa mwaka 2020 uliofanywa na Chuo Kikuu cha Pennsylvania umeiweka REPOA katika nafasi ya 4 kwa ubora katika ya taasisi 92 za utafiti zilizo chini ya jangwa la Sahara zilizoshirikishwa. Ushirikiano wa serikali ya Tanzania na msaada wa washirika wa maendeleo kwa REPOA umewezesha mchango huu mkubwa wa REPOA kwa miaka 25 iliyopita. Washirika wakubwa wa REPOA kwa miaka hii 25 kwa vipindi tofauti ni balozi za nchi za Uholanzi, Denmark, Sweden, Norway, Ireland, Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza, na Shirika la Maendeleo la Utafiti la Canada. Miaka mingine ya ushirikiano wa aina hii ni muhimu, na uwekezaji zaidi kwenye utafiti unahitajika kutoka sekta za umma na binafsi ili tafiti huru na za kuaminika ziendelee kufanyika katika miaka ijayo.




**Waandishi wahabari waandamizi wakifuatilia mafunzo yaliyoandaliwa kwa ajili yao ili kujifunza namna bora ya kuandika matokeo ya tafiti zinazotolewa na REPOA.**